KULEA MIITO MITAKATIFU

Kwa mujibu wa **Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI)**, neno **mwito** *(nomino)* linamaanisha:

👉 **kuita au mwaliko** unaotolewa kwa mtu au kikundi cha watu ili wafanye jambo fulani, waitikie jambo, au wahudhurie tukio.

Kwa **Kanisa Katoliki**, neno **" mwito"** lina maana ya:
kutambua, kusikiliza, na kuitikia wito (mwito) wa Mungu katika maisha ya mtu. **Mwito (miito)** ni mwaliko wa Mungu kwa mtu kuishi maisha fulani au kutumikia kwa namna fulani

Aina za miito katika Kanisa Katoliki

- **Mwito wa upadre (padri)**
- **Mwito wa utawa (masista/ndugu wa kitawa)**
- **Mwito wa maisha ya useja kwa ajili ya huduma**
- **Mwito wa kumtumikia Mungu katika kazi na maisha ya kawaida**

Kwa mujibu wa **Mtg II wa Vat. Hati no 8,** inayohusu **"Dikrii juu ya malezi ya waseminari"** yaani **(Optatam totius)** fungu no 773 inasisitiza kuwa;

Wajibu wa kukuza miito mitakatifu ni wajumuiya nzima ya kikristo na inatakiwa kuutekeleza hasa kwa kuishi Maisha bora ya kikristo. Mchango mkubwa unatolewa na familia zikiongozwa na roho ya Imani. Upendo na uchaji wa Mungu , ambazo hufanywa kama ndio seminari ya kwanza, na vilevile na parokia zenye uhai tele ambazo vijana wenyewe wanashiriki, Walimu na wote ambao kwa namana moja au nyingine, wanahusika kutoa malezi kwa Watoto na vijana haswa katika vyama vya kikatoliki wakijitahidi kuwafundisha vijana waliokabidhiwa ili kutambua wito mtakatifu na kuufuata kwa hiari.

Mapadre wote watakiwa kuonyesha juhudi zao za kitume katika kuiendeleza miiito mitakatifu zaidi iwezekanavyo na kuivutia mioyoya vijana waume kupenda upadre kwa Maisha yao ya upole, yenye bidi wanayoishi kwa furaha Pamoja na mifano ya upendo kati yao na Mapadre na ushirikiano kwa kindugu.

Malezi ya kiroho na kielimu katika seminari ndogo

778 3. Katika seminari ndogo ambazo zimeundwa kuotesha mbegu za wito, wanafunzi wanatakiwa kutayarishwa kwa malezi pekee ya kidini na haswa kwa uongozi wa kiroho wa kufaa, kufuata kristo mkombozikwa roho pendevu ya mioyo mikunjufu.